LUKENYA UNIVERSITY

ISSN 2663-3183 MULTIDISCIPLINARY JOURNAL (LUMJ)

Vol 3, (1), p. 21-27

**Nduni za Fasihi ya Watoto Katika Uwasilishaji wa Dhamira: Kielelezo cha *Sungura Mpanda Ngazi* na *Sitaki Iwe Siri***

**Mutwiri Fred John and *Dkt. Dorcas Musyimi***

*Kikuu cha Chuka, S.L.P 109 CHUKA 60400*

mutwirijfred71@gmail.com

musyimidorcas@yahoo.com

Article history
Received: July 6, 2023
Received in revised form: February 1, 2023
Accepted: February 2, 2023
Available online: https://research.lukenyauniversity.ac.ke/

## IKISIRI

Fasihi ya Kiswahili ya watoto kama taaluma haina muda mrefu katika historia ya fasihi ya Kiswahili. Ikilinganishwa na fasihi ya watu wazima ambayo ilianza muda mrefu, na pia tafiti nyingi kufanyika katika mataifa mengi. Fasihi ya watoto inaonekana kuwa imetelekezwa kwa muda mrefu kutokana na kutokupewa umuhimu unaostahili na wahakiki na hivyo kudharauliwa na wanajamii (Bakize, 2013). Wanajamii wengi wamekuwa wakiinasibisha fasihi hii na mambo ya kitoto ambayo ni rahisi, yasiyo ya msingi sana; na ndiyo maana inaitwa fasihi ya watoto (Wamitila, 2008). Tafiti zinaonyesha kwamba fasihi hii imechipuka barani Afrika hivi karibuni, hasa kwenye miaka ya 1980 kutokana na sababu kadhaa lakini mojawapo ikiwa ni kutiliwa mkazo kwa masuala ya haki za watoto (Ngugi, 2016a). Mulokozi katika Semzaba (2008) anaeleza kwamba nchini Tanzania, fasihi ya watoto ilichipuka wakati na baada ya ukoloni katika miaka ya 1960 na kushika mizizi miaka ya 1970. Zaidi ya hayo, fasihi hii ilishika mizizi zaidi miaka ya 1990 baada ya kuzinduliwa kwa mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania. Nchini Kenya, fasihi ya watoto imepata umaarufu miaka ya 2000 baada ya kujumuishwa katika somo la Kiswahili kuanzia shule ya msingi hadi sekondari. Vilevile, hatua ya serikali ya kugharimia masomo imechangia sana katika maendeleo haya kwa sababu serikali ilichukua jukumu la kununua vitabu vya ziada na kiada. Makala haya yanalenga kutathmini ndumi za fasihi ya watoto kwa kurejelea maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ya watoto kwa kufanya ulinganishi katika nchi za Tanzania na Kenya. Nchi hizi

zimeteuliwa kwa sababu, kwa mujibu wa utafiti wa awali, fasihi ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na fasihi ya watoto ya Kiswahili imepamba moto zaidi katika nchi hizi mbili za Afrika Mashariki kuliko nchi nyingine.

**Istilahi Muhimu:** Dhamira, Nduni, Watoto, Uhalisia.

## 1.0 UTANGULIZI

Fasihi ya watoto ni fasihi inayowalenga watoto pekee. Sign na wenzake (2002) wanaonyesha kuwa fasihi ya watoto ni ile ile moja ulimwenguni kote. Wanasema kuwa ni lazima fasihi hii iwe inaonyesha matendo na maisha ya mhusika kinaganaga, mhusika awe anatia hamasa na lazima iwe inaburudisha. Fasihi ya watoto ni uwanja ambao huhusisha aghalabu kila mtu katika jamii kwani kila mtu huwa na uhusiano wa aina fulani na watoto.

Kulingana na Stephens (1992) fasihi ya watoto hutumika kuingilia katika maisha ya watoto kwani kila jamii huchukulia kuwa utoto ni hatua muhimu katika maisha ya binadamu. Anasema kuwa fasihi yoyote ya watoto huwa na itikadi na hivyo hutumika kama mwongozo wa mtoto katika kumfunzia maadili na thamani ya jamii husika. Mara nyingi mambo ambayo hutokea katika jamii huwa yanaandikiwa watu mbalimbali wakiwemo watoto.

Fasihi ya watoto inatambulika kutokana na sifa maalumu zinazoitofautisha na aina nyingine za fasihi. Sifa kuu ya fasihi ya watoto ni kuwa inalenga hadhira ya watoto. Nodelman & Reimer (2003) wanaeleza kuwa fasihi ya watoto ni aina ya fasihi ambayo kimsingi hadhira yake ni watoto. Naye Bakize (2014) anatoa maelezo sawa na haya lakini kwa kufafanua watoto hasa ni akina nani. Anaeleza kuwa, fasihi ya watoto ni fasihi maalumu inayolenga watu ambao wana umri ulio chini ya miaka kumi na minane. Hivyo, istilahi 'Fasihi ya Watoto' inatokana na uainishaji wa fasihi kwa kuzingatia hadhira. Hata hivyo, chukulizi iliyopo katika fasili hizi ni kuwa, fasihi hii ya watoto imetungwa na watu wazima. Katika miaka ya 2000, watoto wameanza kutunga fasihi yao. Kuna vitabu kadhaa vya hadithi vilivyochapishwa ambavyo vimetungwa na watoto wenyewe wakiwaandikia watoto wenzao.

Kwa mujibu wa Lynch Brown na Carol (1999), tanzu hizo ni kama vile masimulizi ya hadithi, nyimbo za watoto, mashairi ya watoto, semi kama vile vitendawili na maigizo mepesi yanayowalenga watoto. Tanzu hizi zinahusisha fasihi simulizi ya watoto. Tanzu za fasihi andishi ya watoto ni kama vile vitabu vya hadithi za watoto wa viwango mbalimbali kiumri, mashairi mepesi ya watoto na tamthilia. Lundin (2004) anaeleza kuwa, fasihi ya watoto inaendelea kupanuka na kujumuisha filamu za watoto na vipindi vya redio na televisheni vya hadithi za watoto. Ingawa utafiti huu unarejelea fasihi ya watoto kwa jumla, hasa ulichunguza vitabu vya hadithi za watoto kama utanzu wa fasihi andishi ya watoto.

## 2.0 MATOKEO

### 2.1 Sifa za Kiwahusika

Lynch-Brown na Carol (1999) wanaeleza kuwa wahusika ni 'waigizaji' katika kazi ya fasihi. Naye Wamitila (2016) anaboresha fasili hii kwa kutoa kauli kuwa wahusika ni viumbe katika hadithi. Mwanafasihi huwabuni wahusika na kuwaweka katika mandhari ambayo yatafanikisha ufikiaji wa maudhui anayokusudia kutokana na vitendo anavyowafanyisha wahusika, maneno anayowasemesha na jinsi anavyofanya watagusane. Bakize (2014) anaeleza kuwa

ingawa hadhira ya watoto huvutiwa na hadithi zenye wahusika wanyama, wengi wao hupendelea hadithi kuhusu binadamu hasa zile zenye wahusika wa rika lao. Ikiwa hadithi ni ya wahusika wanyama huvutiwa nayo hasa ikiwa wale wanyama wanatenda matendo ya kibinadamu na hivyo kuwakilisha watu ambao wasomaji wanaweza kujinasibisha nao.

Ni muhimu hadithi iwe na wahusika mseto wa wavulana na wasichana na kadri iwezekanavyo isawiri usawa wa kijinsia ambapo hakuna mhusika anayesawiriwa kama duni kutokana na jinsia yake. Inapendekezwa na wataalamu kama vile Lynch-Brown na Carol (1999) kuwa wahusika wakuu ambao ni watoto wawe na umri unaolingana na wa watoto wanaolengwa katika hadithi husika. Bakize (2014) anaendelea kueleza kuwa, japo fasihi hii huhusisha wahusika wa aina nyingine wakiwemo wanyama, mazimwi na hata watu wazima hapa na pale, wengi wa wahusika hasa wahusika wakuu huwa ni watoto wenyewe ili kuweza kuvutia hadhira lengwa.

*Sungura Mpanda Ngazi* ni hadithi ambayo imesukwa kwa kutumia wahusika wanyama. Kulingana na Bakize (keshatajwa) watoto huvutiwa sana na hadithi zenye wahusika wanyama. Watoto hufurahishwa na hadithi zinazorejelea wanyama ambao huchukua nafasi ya binadamu na ambao watoto wanaweza kujinasibisha nao.

*Sungura Mpanda Ngazi* ni hadithi iliyotumia wahusika wanyama. Wanyama hawa wanakabiliwa na njaa wasipate chochote cha kula. Hata hivyo, kuna maembe kwenye mwembe mrefu sana. Ni baada ya kutafakari, Sungura anaibua wazo la kuunda ngazi ili apande juu kuwaangushia wanyama wenzake maembe. Anapofika juu, sungura anakulamaembe na kuwasahau wanyama wenzake wanaomsubiri chini ya mwembe.

Sungura kwa sababu ya tamaa anapopanda anasahau wanyama wengine. Swara anateta *"Sisi tulikusaidia kwa roho safi upande. Tulitarajia utatusaidia kwa kutuangushia maembe mabivu. Hata maembe mabichi umekataa katakata kutuangushia. Sasa umetutema kama masuo". Ngiri aliongezea "Ndugu Sungura hata kama umefika huko kileleni, kumbuka huwezi kukaa mwembeni daima. Natumai unakumbuka, mpanda ngazi hushuka."*

*Sungura Mpanda Ngazi* (uk16).

Mwandishi kwa kutumia wahusika wanyama wanaowavutia watoto amefanikiwa kuwasilisha dhamira yake kwa watoto. Mwandishi anadhamiria kufunza watoto athari za tamaa. Umuhimu wa kushirikiana katika jamii ni suala ambalo ni muhimu kwani Sungura asingeweza kutengeneza ngazi akiwa pekee yake. Sungura anapokosa kuwapa wanyama wenzake maembe wanaamua kuondoa ngazi iliyomwezesha Sungura kupanda, jambo linalosababisha kifo cha Sungura. Ama kwa kweli mwandishi amefanikiwa kuwafunza watoto pamoja na watu wazima wanaosoma kazi hii kuwa, tamaa mbele mauti nyuma.

**2.2 Sifa za Picha**

Picha katika hadithi za watoto ni kipengele cha mtindo. Mwandishi hutumia picha kama nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa watoto wanaolengwa. Lynch-Brown na Carol (1999) wanaelekeza kuwa picha katika fasihi ya watoto zihusishe jinsia zote mbili yaani kike na kiume ili watoto wote wanaosoma waweze kuvutiwa na hadithi zenyewe kwa kujiona ndani mwa hadithi. Bakize (2014)

naye anaeleza kuwa picha zinafaa ziambatane na kiwango cha hadhira ya watoto wanaolengwa kusoma hadithi husika. Kwa mfano, kitabu kinachokusudiwa kusomwa na watoto wa miaka kumi kiwe na picha zinazosawiri watoto wa miaka kumi.

Katika hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi* ukurasa wa pili mwandishi amechora picha ya mwembe wenye maembe mengi mabivu na mengine mabichi. Kuna wanyama kama vile fisi anayetokwa na mate kwa ajili ya tamaa. Fisi anatoa wazo kuwa watafute mawe wapige yale maembe na yale ya kwanza kuanguka fisi anapendekeza yawe yake. Wengine wanamcheka kwa tamaa ya kujifikiria kwanza. Kutokana na picha hizi mwandishi amefanikisha dhamira yake kwani kupitia kwa picha hizi zinazowavutia walengwa yaani watoto huwavutia na kuwa na shauku ya kutaka kujua kinachozungumziwa katika nakala hiyo. Kuna picha ukurasa wa saba unaoashiria ushirikiano kati ya wanyama hawa. Wote wamebeba miti ili kufanikisha pendekezo la Sungura la kutengeneza ngazi ya kuwawezesha kupata maembe.

Katika ukurasa wa kumi na mbili kuna picha ya Sungura ambaye ameanza kula maembe na kuwasahau wenzake. Macho ya wanyama wenzake yanamtazama. Sungura anangusha ganda baada ya kula huku wanyama wengine wakifikiria kuwa ni embe. Wanang'ang'ania kabla ya kugundua kuwa lilikuwa ganda. Katika ukurasa wa 21 wanyama wanakasirika na kuharibu ngazi iliyomwezesha Sungura kupanda kisha wakaondoka. Matokeo yake yamesawiriwa na mwandishi katika ukurasa wa 26 ambapo Sungura anajuta na majuto ni mjukuu baada ya kugundua bila shaka kuwa mpanda ngazi sharti ashuke. Sungura anaangamia kutokana na tamaa yake.

**2.3 Sifa za Rangi**

Matumizi ya rangi ni kipengele cha mtindo katika fani kwa kuwa ni nyenzo inayotumiwa na mwandishi wa hadithi kuwasilisha ujumbe kwa mtoto msomaji. Lynch-Brown na Carol (1999) wakiandika kuhusu rangi katika fasihi ya watoto wanasema kuwa rangi inachangia mvuto na hisia za mtoto katika kitabu. Matundura (2007) anaweka wazo hili katika muktadha wa matumizi na kueleza kuwa hadithi za watoto huwa na picha zenye rangi za kuvutia. Picha hizi huwasilisha ujumbe kwa mtoto kwa njia ya kutazama badala ya kusoma masimulizi. Ngugi (2014) anakuza hoja hii na kueleza kuwa mbali na picha katika fasihi ya watoto kuwa angavu na yenye mvuto, rangi ya karatasi na utoaji wa kitabu kizima ni muhimu. Rangi ya karatasi pia inafaa iwe angavu na rangi zilizotumiwa ziwe na uhalisia.

Katika *Sungura Mpanda Ngazi*, picha zote ni za mazingira yale yale ambapo ni mahali chini ya mwembe, rangi ya kijani kibichi ya mwembe imetumika kuonyesha hali halisi ya mazingira yanayomzunguka msomaji. Rangi ya samawati, nyekundu na kijivu zimetumika ili kumvutia msomaji na kumpa mnato wa kutaka kusoma kazi hii ya *Sungura Mpanda Ngazi.* Kadhalika, picha katika *Sungura Mpanda Ngazi*, zina msisitizo wa rangi ya kijani kibichi. Rangi hii inahusishwa na majani yaliyo katika mazingira ambayo yana mvua ambayo inanawirisha majani yakaendelea kuwa na rangi hiyo inayohusishwa na ustawi wa kilimo. Usawiri huu unampa msomaji ambaye ni mtoto taswira kamili ya mazingira anamoishi na hivyo kuelewa kwa upesi kwa mtoto anayesoma kazi hii.

Katika jalada la hadithi ya Sungura Mpanda Ngazi mada hii imeandikwa kwa herufi kubwa na kwa rangi ya kuvutia ya manjano. Mtoto atavutiwa na rangi hii na kutaka kusoma nakala hii. Mwandishi vilevile, ametumia rangi nyekundu kusisitiza maneno fulani. Kwa mfano ukurasa wa 5 mwandishi amekolesha msemo "waliwaza na kuwazua" kuonyesha jinsi ambavyo wanyama hawa walikuwa na tatizo mbele yao la kubaini njia ya kupata maembe kutokana na njaa iliyosababishwa na kiangazi. Kila nambari ya ukurasa imekoleshwa rangi nyekundu hii ni rangi mojawapo zinazowavutia watoto na kuwawezesha kusoma hadithi.

**2.4 Sifa za Kimuundo**

Pinnel na Fountas (2006) wakieleza jinsi vitabu vya fasihi ya watoto vinavyofaa kuandikwa, wanaeleza kuwa vinafaa kuwa vifupi na sentensi pia ziwe fupi na zenye miundo sahili ili ujumbe uweze kueleweka moja kwa moja na bila matatizo kwa kuwa urazini wa watoto huwa mdogo. Aidha, anwani fupi ni bora kuliko anwani ndefu kwa vile hukumbukika kwa wepesi. Mtoto ataweza kukumbuka haraka hadithi aliyosoma ikiwa atakumbuka anwani. *Sungura Mpanda Ngazi* ni anwani iliyo na maneno matatu tu.

Hii inasaidia mtoto kukumbuka anwani hii kwa wepesi. Mada ya fasihi ya watoto pia inapaswa kuwa ya kuvutia. Mwandishi anapoipa hadithi mada ya *Sungura Mpanda Ngazi* inamvutia msomaji na kumpa taharuki ya kutaka kujua mbona kwa nini Sungura apande ngazi. Aidha, ni nini kinachofanyika baada ya kupanda ngazi. Ni kutokana na mvuto wa kutaka uvumbuzi wa maswali haya mwandishi anafanikisha dhamira yake mtoto anaposoma na kuona tamaa ya Sungura inayomfanya kusahau wanyama wenzake waliomwezesha kupanda mwembe kwa kumtengenezea ngazi. Matokeo ya tamaa ya Sungura yanasababisha kifo chake.

Sentensi alizotumia mwandishi wa *Sungura Mpanda Ngazi* ni sahili. Kwa mfano ukurasa wa 13 aya ya pili. *"sungura alimjibu kwa maringo, "Maembe ni yangu. Hakuna mkataba wa maelewano tulioandikiana kuwa nikiwa juu niwaangushie maembe." Wanyama hawakuamini maneno ya sungura. Walifikiri wanaota mchana. Swara akamwuliza Sungura, "Ati wasema nini?" Sungura akajibu kwa madaha zaidi, "kama masikio yenu yana pamba, itoeni ili msikie vizuri. Nimesema na ninarudia, maembe ni yangu. Hakuna mkataba wa maelewano tulioandikiana kuwa nikiwa juu niwaangushie maembe."* Katika kifungu hiki ni dhahiri kuwa idadi kubwa ya sentensi alizotumia mwandishi katika kazi hii ni sentensi sahili. Mwandishi ana ufahamu kuwa watoto hawana urazini wa kuelewa sentensi ndefu kama ambatano na hivyo kutumia sentensi sahili kurahisisha mawasiliano yake na mtoto.

**2.5 Sifa za Kimsamiati**

Kilichochunguzwa kuhusu msamiati hapa ni kiwango cha msamiati uliotumika katika hadithi za watoto zilizoteuliwa. Ngugi na Nabea (2011) watoa hoja kuwa ili vitabu vya hadithi za watoto viweze kufanikiwa, lazima viwe sahili kifani na vya moja kwa moja kulingana na umri wa watoto wanaolengwa kuvisoma. Kimsamiati, lugha ya fasihi ya watoto huwa na wepesi unaotegemea kiwango cha ukuaji wa watoto kiumri na pia kiakili ili mtoto atakayesoma aweze kuifuata hadithi na kufikiwa na ujumbe wake kwa wepesi. Hadithi ya *Sungura Mpanda Ngazi* imetumia msamiati sahili kuwasilisha ujumbe na dhamira ya mwandishi. Kwa

mfano: maelezo ya mwandishi ukurasa wa kwanza ni wa moja kwa moja. *Wanyama walikuwa wamekusanyika chini ya mwembe. Mwembe ulikuwa na maembe mabivu na mabichi. Lakini maembe yaliyowavutia wanyama zaidi ni yale mabivu.*

*Hata hivyo, hawakuwa na namna ya kuyafikia. Mwembe ulikuwa mrefu ajabu. Mwembe ulikuwa na utelezi. Kila mnyama aliyejaribu kuukwea, aliteleza na kuanguka. Nusura wakate tamaa. Ilikuwa ni kama kuwa na wali, kisha ukose kijiko. Wanyama kama fisi walidondokwa na mate walipoona maembe mabivu yakining'inia kwenye mwembe. Fisi alijaribu kuukwea mwembe. Aliteleza na kuanguka. Aliumia mguu wake wa mbele. Alianza kutembea akichechemea.*

Maelezo haya ni ya kisahili. Msamiati uliotumika ni rahisi kueleweka na mtoto anaposoma kazi hii. Wepesi wa lugha humwezesha mwandishi kuwasilisha dhamira yake kwa upesi kwani watoto huelewa hadithi kwa upesi. Misamiati na mtindo uliotumika ni wepesi. Msemo kama vile, wanyama karibu wakate tamaa ni rahisi kueleweka na watoto kwani unaelezea jinsi wanyama walivyoshindwa kuukwea ule mwembe kupata maembe.

### 2.6 Sifa za Kimandhari

Mandhari, kama wanavyofasili Lynch-Brown na Carol (1999), ni mahali na wakati wa tukio. Wanaeleza kuwa mandhari ya hadithi za watoto aghalabu huwa ni mazingira ambayo yanahusishwa na shughuli au matendo ya watoto na maisha yao ili watoto halisi wanaosoma hadithi husika waweze kujitambulisha nazo. Mazingira haya ni kama vile shuleni, nyumbani, uwanjani na njiani. Haya ni mandhari yanayofahamika kwa urahisi na watoto kwa kuwa watoto mara nyingi huwa katika shughuli za nyumbani au za shuleni. Mwandishi wa *Sungura Mpanda Ngazi* amezua mandhari ya shamba. Mandhari ambayo kila mtoto anayafahamu kwani nyumbani kuna mashamba ambayo hutumiwa kulimia mimea na mitunda mbalimbali kama vile maembe. Mandhari aliyochora mwandishi wa *Sungura Mpanda Ngazi* ni mazingira yanayomvutia mtoto. Watoto hufurahi kwenda shambani kula matunda. Mandhari haya humvutia msomaji na kumpa mvuto wa kusoma kwani mandhari yaliyowasilishwa kwa mtoto ni halisi. Ukurasa wa kwanza tunaarifiwa kuwa wanyama walikuwa wameketi chini ya mwembe ambao ulikuwa na maembe mabivu na maembe mabichi.

## 3.0 HITIMISHO

Katika makala hii, nduni za fasihi ya watoto zimechunguzwa, kubainishwa na kufafanuliwa. Makala imefafanua dhana ya fasihi ya watoto na nduni za fasihi ya watoto. Mjadala katika makala hii umebainisha kuwa lazima fasihi hii iwe inaonyesha matendo na maisha ya mhusika kinaganaga, mhusika awe anatia hamasa na lazima iwe inaburudisha. Makala haya yameweka wazi nduni za fasihi ya watoto zinazotumika kubainisha fasihi ya watoto amabazo ni pamoja na; Sifa zawahusika; ni muhimu hadithi iwe na wahusika mseto wa wavulana na wasichana na kadri iwezekanavyo isawiri usawa wa kijinsia ambapo hakuna mhusika anayesawiriwa kama duni kutokana na jinsia yake. Sifa za picha; picha katika hadithi za watoto ni kipengele cha mtindo. Mwandishi hutumia picha kama nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa watoto wanaolengwa. Sifa za rangi; matumizi ya rangi ni kipengele cha mtindo katika fani kwa kuwa ni nyenzo inayotumiwa na mwandishi wa hadithi kuwasilisha ujumbe kwa mtoto msomaji. Sifa

za kimuundo; sifa za kimsamiati na sifa za kimandhari zimefafanuliwa kufanikisha malengo ya makala hii.

**MAREJELEO**

Akinyemi, A. (2003). Yoruba Oral Literature: A Source of Indigenous Education for Children. In Akin Oyatede (ed). *Journal of African Studies*. Volume 16, Number. 2, December 2003.

Birketveit, A (2006). *Self Interpretation and Ideology in Children's Literature.* Bergen University College.

Brunner, J. (2003). *Making Stories. Law, Literature, Life*. Cambridge, London: Harvard University Press.

Chimerah, R. & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Knowles, M. & Malmkjær K. (1996). *Language and Control in Children's Literature*. London/New York: Routledge.

Kobia, J. (2008). *Sungura Mpanda Ngazi.* Nairobi: KLB.

Komora, Y. (1971). *Usininyonye*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Marx, K. & Engels, F.(1998) *The German Ideology*: *Literary Theory* Oxford: Blackwell Publishers.

Matundura, B. (2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto.Unpublished M.A. Thesis. University of Nairobi.

Muriungi, C.K (2006). Emerging Trends in Kenya Childrens's Fiction: A study of Sasa Sema's Lion Books. Published, PhD. University of Witwatersrand. Johannesburg.

Ngugi, P. (2009). Language and Literary Education: The State of Children's Literature in Kiswahili in Primary Schools in Kenya, Ph.D. Thesis. University of Wien.

Njoroge, N. (1978). *African Oral Literature: Fighting Literature*. In Eddah Gachukia & Akivaga Kichamu (eds.) *Teaching of African Literature in Schools.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.